

Tufani za Majira ya Baridi

Wakati wa tufani ya majira ya baridi, kunaweza kuwa na baridi, upepo, na theluji. Tufani ya majira ya baridi inaweza kuwa ya muda wa masaa machache mpaka siku kadhaa. Fuata maelekezo haya ili uwe salama.

Kama tu unavyopiga simu kwa 9-1-1 kwa msaada kuhusu mtu aliyeumia au aliyehatarini, unaweza kupiga simu kwa 2-1-1 ili upate maelezo ya kusaidia na matatizo mengine, kama vile matatizo ya hali ya anga. Dayo 2-1-1 kwenye simu yako na useme lugha yako. Kuna mtu atakaye kusaidia maswali yako kwa lugha yako.

Jitayarisha.

Hadhari ya Tufani ya Majira ya Baridi humaanisha huenda kukawa na hali ya anga ya majira mabaya sana ya baridi siku moja au mbili zifuatazo.

Ilani ya Tufani ya Majira ya Baridi humaanisha kwamba hali ya anga ya majira makali ya baridi yanakuja au tayari yako hapa.

Ushauri wa Hali ya Anga ya Majira ya Baridi humaanisha kwamba hali ya anga ya majira ya baridi yanaweza kufanya uendeshaji gari au kutembea nje vigumu au hatari.

Ilani ya Dhoruba Kali ya Theluji humaanisha kwamba thluji na upepo mkali utafanya kuwe na baridi sana nje na kuwe vigumu kuona.

Ilani ya Jalidi/Kufrizi humaanisha kwamba halijoto za kufrizi zinakuja ambazo zinaweza kudhuru mimea na mazao.

Sikiliza redio.

- Sikiliza stesheni ya redio ya _____ kwa maelezo ya lugha yako. Endelea kusikiliza mpaka usikie lugha yako ili ujue kinachoendelea na unachopaswa kufanyana. – AU –
- Kuwa na mtu anayeelewa Kiingereza asikilize redio ili ujue kinachoendelea na unachopaswa kufanya.

Kuwa salama wakati wa tufani za majira ya baridi.

Nyumbani:

- Kaa nyumbani kama unaweza.
- Umeme unaweza kupotea. Kuwa na chakula na maji yatakayotosha siku chache kama huwezi kutoka nyumbani.
- Kama uko na simu ya mkononi, ichaji kabisa.
- Usitumie majiko ya kupikia nje ndani. Yanaweza kutoa gesi ambazo zinaweza kukudhuru au kukuuu.
- Wacha maji yamwagike kwa sinki na hodhi zako ili mifereji isigande.
- Kama utakosa joto kabisa au uko na matatizo yoyote mabaya nyumbani dayo 2-1-1.

Nje:

- Kama lazima uende nje, vaa mavazi ya joto yanayofunika mwili wako wote.
- Vaa mavazi kadhaa yenye joto. Vaa kofia. Funika mdomo na pua yako na skafu. Weka miguu yako ikiwa imekauka. Vaa soksi za sufu.
- Kagua mwili mara kwa mara kuangalia kama kuna ngozi au sehemu zilizoganda. Ngozi iliyokauka haitakuwa tofauti na huenda isiwe na hisi zozote, na huenda ikawa na ugumu wa kusongea. Ukiona uko na ngozi au sehemu ya mwili iliyokauka, nenda ndani na uipashe joto pole pole. Usisugue sehemu zilizoganda.

- Kuwa makini ukitembea nje. Njia za kando huenda zikawa na theluji na za kuteleza.

Ndani ya gari:

- Kama lazima uendeshe gari, kuwa makini sana. Inachukua gari muda mrefu kusimama kwenye barabara zenye theluji. Endesha gari pole pole, na weka umbali zaidi kati ya gari lako na gari lililo mbele yako.
- Piga breki kwa upole kwenye barabara iliyo na theluji. Kama magurudumu yataaza kukwama, wachilia breki pole pole.
- Washa mataa ya gari lako ili magari mengine yakuone.
- Weka tenki la mafuta ya gari likiwa limejaa ili mafuta yasigande.
- Weka vifaa vya dharura ndani ya gari lako: blanketi, tochi, maji ya kuosha kioo cha mbele, kikwaruzo cha kioo cha mbele, na waya za kushtua gari, chakula na maji.
- Kama gari lako litakwama katika theluji mbali na usaidizi, usitembee kutafuta msaada. Ni salama zaidi kungojea msaada ndani ya gari. Kama unahitaji kuwasha joto, hakikisha kwamba bomba la ekzosi halijafunikwa na theluji. Kama hakuna mtu yoyote karibu, piga simu utafute msaada.

Tufani ya Majira ya Baridi • Kiingereza • Mei 2012